

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**KIKAO CHA KUMI NA TATU**

**13 FEBRUARI, 2025**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 13 FEBRUARI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

##### **215. MHESHIMIWA BERNADETHA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, asilimia ngapi ya Waajiri nchini wamejiunga na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na unawanufaishaje Wafanyakazi.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **216. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Mradi wa TACTIC Tire II utaanza na ni lini unatarajiwa kukamilika kwenye Manispaa zinazohusika.

#### **OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

##### **217. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Wananchi watarajie nini baada ya kumalizika kwa Mradi wa TASAF.

#### **WIZARA YA NISHATI:**

##### **218. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha bei ya Shilingi 27,000/= kuunganisha umeme kwa Wananchi walioshindwa kulipia Shilingi 320,000/=.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**219. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itatafuta Wawekezaji wa Viwanda vidogovidogo vya kuongeza thamani katika Zao la Ndizi.

## **WIZARA YA MAJI:**

**220. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itachimba visima virefu vya maji kwenye Taasisi za Umma hususani mashulenii.

**221. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuvilinda na kuvihifadhi vyanzo vya maji nchini kwa kuzihusisha Sekta za Misitu, Kilimo na Mifugo.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **222. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni haja ya kukipatia Chuo cha SUA Tawi la Tunduru eneo la Kiwanda cha kubangua Korosho kilichotelekezwa.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **223. MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Korogwe TC litapatiwa Gari jipya la Zimamoto.

## **V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

## **VI. HOJA ZA KAMATI:**

### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**DODOMA  
13 FEBRUARI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**

